

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA



Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na. CDC/S.10/4/15

Tarehe. 21/07/2022

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anapenda kuwataarifu Waombaji Kazi wote walioomba kazi ya katika kada ya Udereva, Msaidizi wa Kumbukumbu II, Katibu Mahsusi na Mtendaji wa Kijiji kuwa usaili unatarajiwa kuendeshwa kuanzia tarehe 28/07/2022 hadi tarehe 02/08/2022 na hatimaye kuwapangia vituo vya kazi waombaji kazi watakaofaulu usaili huo.

Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia tarehe na maelekezo mengine kama ifuafuatayo:-

UDEREVA

- Tarehe ya Usaili wa Mchujo ni 28/07/2022.
- Tarehe ya Usaili wa Vitendo ni 29/07/2022
- Tarehe ya Usaili wa Mahojiano ya Ana kwa ana ni 30/07/2022

KATIBU MAHSUSI

- Tarehe ya Usaili wa Mchujo ni 28/07/2022.
- Tarehe ya Usaili wa Vitendo ni 29/07/2022
- Tarehe ya Usaili wa Mahojiano ya Ana kwa ana ni 30/07/2022

MTUNZA KUMBUKUMBU

- Tarehe ya Usaili wa Mchujo ni 31/07/2022.
- Tarehe ya Usaili wa Mahojiano ya Ana kwa ana ni 01/08/2022

MTENDAJI WA KIJIKI

- Tarehe ya Usaili wa Mchujo ni 31/07/2022.
- Tarehe ya Usaili wa Mahojiano ya Ana kwa ana ni 01-02/08/2022

Muda wa Usaili ni kuanzia saa mbili kamili aubuhi (2:00), Mahali ni Katika Ukumbi wa Halmashauri (Sapanjo).

Itigi Road, S.L.P73, Chunya simuyamezani: 025 2520121,Baruapepe: ded@chunyadc.go.tz,
tovuti:www.chunyadc.go.tz

- i. Kila msailiwa anatakiwa kufika kwenye eneo la usaili akiwa amevaa Barakoa
- ii. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi;
- iii. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha Mpiga kura, Kitambulisho cha kazi, Leseni ya Udereva ,Kitambulisho cha Uraia Hati ya kusafiria au barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Mtendaji iliyo na Picha (passport size);
- iv. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **VYETI VYAO HALISI**, kuanzia cheti cha kuzaliwa, kidato cha IV, VI, Stashahada, Stashahada ya Juu, Shahada , Leseni ya Udereva na kuendelea kutegemeana na sifa za Mwombaji; Watakaofika nan akala za vyeti hawatapokelewa na hawataruhusiwa kuendelea na usaili.
- v. Wasailiwa watakaowasilisha “**Testimonials**”, “**Provisional Results**”, “**Statement of results**”, hati za matokeo za kidato cha IV na VI (form V and form VI results slips) **HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI**;
- vi. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi;
- vii. Kila Msailiwa azingatie tarehe, muda na mahali alipopangiwa kufanyia usaili;
- viii. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (kama TCU, NACTE au NECTA);
- ix. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo, wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya tangazo husika;
- x. Matumizi ya simu hayaruhusiwi wakati wa usaili.